


KITARU CHA
AGANO JIPYA

LA



BWANA NA MWOKOZI WETU

ISA MASIYA.

KIMEFASIRIKA KATIKA MANENO YA KWANZA YA KIYONANI.

3292

LONDON :
KIMEPIGWA CHAPA KWA BRITISH AND FOREIGN
BIBLE SOCIETY.

—
1883.

ANJILI KWA MATTAYO.

KITABU cha kizazi chake Isa Masiya, mwana wa **1**
Daúd, mwana wa Ibrahimu.

Ibrahimu alizaa Isaak, Isaak akazaa Yakób, Yakób **2**
akazaa Yuda na ndugu zake. Yuda akazaa Farez na Zara **3**
kwa Tamar, Farez akazaa Hesrón, Hesrón akazaa Arám, **4**
Arám akazaa Aminadáb, Aminadáb akazaa Nahashón, **5**
Nahashón akazaa Salmón, Salmón akazaa Boaz kwa **6**
Raháb, Boaz akazaa Obéd kwa Ruth, Obéd akazaa Yese,
Yese akazaa Mfalme Daúd. **6**

Mfalme Daúd akazaa Sulemán kwake wa Uriya, **7**
Sulemán akazaa Rehabyám, Rehabyám akazaa Abiya, **8**
Abiya akazaa Asa, Asa akazaa Yehoshafát, Yeho-
shafát akazaa Yorám, Yorám akazaa Uziya, Uziya **9**
akazaa Yothám, Yothám akazaa Aház, Aház akazaa **10**
Hezekiya, Hezekiya akazaa Manasse, Manasse akazaa
Amón, Amón akazaa Yosiya, Yosiya akazaa Yekoniya **11**
na ndugu zake wakati walipohamishwa Babél.

Na baada ya kuhamishwa Babél, Yekoniya akazaa **12**
Shealtiel, Shealtiel akazaa Zerubabél, Zerubabél aka- **13**
zaa Abihúd, Abihúd akazaa Eliyakim, Eliyakim akazaa **14**
Azór, Azór akazaa Sadók, Sadók akazaa Ahím, Ahím **15**
akazaa Eliyúd, Eliyúd akazaa Eleazar, Eleazar akazaa **16**
Mattán, Mattán akazaa Yakób. Yakób akazaa Yusuf, **17**
aliye mume wake Maryamu, aliye mzaa ISA, aitwaye
Masiya.

Navyo vizazi vyote tangu Ibrahimu hatta Daúd, vizazi **18**
kumi na vinne; navyo tangu Daúd hatta kuhamishwa
Babél, vizazi kumi na vinne; navyo tangu kuhamishwa **19**
Babél hatta Masiya, vizazi kumi na vinne.

Na kizazi chake Isa Masiya chalikuwa hivi. Walipoa- **20**
hadiana mama yake Maryamu na Yusuf, hawajakari-
biana pamoja, alionekana ana mimba kwa Roho Mtaka-
tifu. Naye Yusuf mumewe, akiwa mwenyi kaki, asitake **21**
kumwaibisha, alithani kumwacha kwa siri. Alipokuwa **22**